

UKAMBI

UKAMBI NI UGONJWA MBAYA

Ukambi ni ugonjwa mbaya unaosababisha upele na homa.

Ukambi ni ugonjwa wa kuambukiza. Unasambaa mtu aliye na ukambi anapopumua, kukohoa au kupiga chafya.

Mtu yeyote ambaye hajachanjwa anaweza kupata ukambi.

Ukambi unaweza kuwa hatari, haswa kwa watoto wachanga. Katika hali nadra, unaweza kusababisha kifo.



LINDA FAMILIA YAKO DHIDI YA UKAMBI

Njia bora ya kulinda familia yako dhidi ya ukambi ni kuchanjwa.

Madaktari wanapendekeza watoto wote wadungwe sindano ya MMR.

Sindano ya MMR ni salama na bora kwa kuzuia ukambi. Pia hulinda dhidi ya matumbwitumbwi na rubela.

Kupata chanjo ya MMR ni salama kuliko kupata ukambi.

Watoto wengi hawana madhara ya kando kutokana na sindano. Madhara ya kando yanayotokea kwa kawaida ni madogo na hayadumu kwa muda mrefu, kama vile homa, upele kidogo na maumivu.



CHANJO YA MMR HAISABABISHA UGONJWA WA AKILI WA WATOTO

Hakuna tafiti ambazo zimepata uhusiano kati ya ugonjwa wa akili wa watoto na chanjo ya MMR. Hili limechunguzwa kwa makini sana na madaktari na wanasayansi wengi kote duniani.

Wanasayansi wanachunguza kinachomfanya mtoto kuwa na uwezekano zaidi wa kupatwa na ugonjwa wa akili. Wanasayansi wengi wanakubali kuwa jeni za familia zinaweza kumfanya mtu kupata ugonjwa wa akili wa watoto. Pia wanachunguza uhusiano kati ya ugonjwa wa akili wa watoto na pale mtu anapoishi.

Mwulize daktari wako ikiwa una maswali kuhusu ukambi au chanjo ya MMR.

UNACHOPASWA KUFANYA IKIWA UNADHANI KUWA UNA UKAMBI

Dalili za ukambi na jinsi unavyosambaa

Mara nyingi ukambi huanza kwa homa ya juu, kikohozi, kamasi na macho mekundu yenye majimaji. Baada ya siku 3-5, kwa kawaida upele huanza usoni na kusambaa hadi sehemu nyingine za mwili.

Unaweza kusambaza ukambi kwa wengine pindi unapokuwa na dalili. Unaweza kuambikizwa hadi pale upele utakapoisha.

Unaweza kupata ukambi kwa kuwa katika chumba ambapo mtu aliye na ukambi amekuwa. Virusi vya ukambi vinasalia hewani kwa hadi saa mbili baada ya mtu huyo kuondoka kwenye chumba hicho.

Wasiliana na daktari au kliniki yako moja kwa moja ukiona dalili

Daktari au kliniki yako itakufahamisha ikiwa unahitaji kuzuru kliniki.

Ukambi unaweza kuambukizwa na unaweza kumpa mtu katika chumba cha kusubiri. Ni muhimu kumwambia daktari au kliniki yako kuwa una dalili za ukambi **kabla** hujaenda. Watakupa maagizo ya unachopaswa kufanya ili usisambaze ukambi.

Kaa nyumbani ikiwa una ukambi

Ni muhimu kutosambaza ukambi kwa wengine.

Kaa nyumbani ikiwa una ukambi. Usiende shuleni, kazini, dukani, wala nyumbani kwa watu wengine.

Usiwaruhusu wageni nyumbani kwako ikiwa wewe au mtoto wako mna homa au upele.